



AINA KUU ZA UDONGO KATIKA MAENEKO YA USUKUMANI

Katena ya udongo (kutoka
mlimani hadi mabondeni)



KUMBUKA:

Aina hizi kuu za udongo hufanyiwa uta-fiti kwa kuchunguzwa mashambani na katika maabarara ili kubaini mapungufu na kutengeneza teknolojia sahihi za kuboresha mabungufu hayo ili kufanya kilimo kiwe endelevu na kutunza maringira kwa ujumla



5. Udongo wa Kichanga ("Luseni")

Sifa za udongo huu

1. Una kina kirefu hadi kirefu sana
2. Unapatikana sehemu zilizo chini ya mlima kuelekea bondeni.
3. Hauhifadhi maji na virutubisho
4. Ni udongo wa kichanga tifutifu hadi tifutifu kichanga.

5. Kwa kawaida udongo huu huwa na pH ya tindikali au asidi.

6. Hustawisha mazao mbalimbali hasa yale ambayo hayahitaji kutuama kwa maji.
7. Rutuba yake ni ndogo hadi ndogo sana.
8. Nirahisi kuulima.
9. Inashauriwa kutumia mbinu hushishi au mchanganyiko ili kuhifadhi ipasavyo rutuba, maji na kuzuia mmomonyoko wa udongo huu na aina zingine za udongo ipasavyo.



Kwa maelezo zaidi wasiiiana na :

Mkurugenzi wa Kituo

TARI - UKiriguru

S. L. P. 1433
Mwanza

Barua pepe:

cdukiriguru@tari.go.tz

Simu : +255 (735) 983 104
+255 (282) 983 104

I. Udongo wa Kichanga chekundu ("Kikungu")



Sifa za udongo huu

1. Una kina kirefu
2. Hupitisha maji kwa urahisi
3. Una rangi nyekundu
4. Ni mfinyanzi hadi mfinyanzi tifutifu
5. Una rutuba kiasi
6. Hauhifadhi maji kwa muda mrefu sana pH yake kwa kawaida ni ya tindikali au asidi.
7. Hustawisha mazao mbalimbali hasa yasiyohitaji kutuuma kwa maji.
8. Hustawisha mazao mbalimbali hasa yasiyohitaji kutuuma kwa maji.



Sifa za udongo huu

- Una kina kirefu
- Hupitisha maji kwa urahisi
- Una rangi ya wekundu
- Ni kichanga tifutifu hadi kichanga mfinyanzi
- Una rutuba ndogo
- Hauhifadhi maji kwa muda mrefu
- Kwa kawaida pH yake ni ya tindikali.
- Hustawisha mazao mbalimbali hasa yasiyohitaji kutuuma kwa maji.

3. Udongo wa Mfinyanzi mweusi ("Mbuga")

Sifa za udongo huu

1. Una kina kirefu
2. Una mfinyanzi mwingu
3. Hupasuka na kutengeneza nyufa kubwa wakati wa kiangazi
4. Kwa kulinganishwa na aina nyingine za udongo, udongo huu una rutuba nzuri.
5. Una rangi nyeusi
6. Hupatikana mabondeni na sehemu za tambareare.
7. Kwa kawaida udongo huu huwa na chumvichumvi au magadi.
8. Ni mgumu kuulima nyakati za mvua na kiangazi.
9. Huhifadhi maji kwa muda mrefu ukiling-anishwa na aina nyingine za udongo.
10. Hustawisha mazao mbalimbali, yakiwemo yale yanayohitaji kutuuma kwa maji mpunga wa mabondeni



4. Udongo wa kichanga chenyé tabaka gumu katika kina ("Itogolo")

Sifa za udongo huu

1. Udongo wa juu ni kichanga tifutifu
2. Udongo wa chini ni kichanga mfinyanzi hadi mfinyanzi mweusi.
3. Unarutuba kiasi.
4. Unatabaka gumu la mfinyanzi ambalo huzuia maji kupenya haraka.
5. Unatuamisha maji kwa sababu ya kuwa na tabaka gumu.
6. pH yake ni ya tindikali hadi alikali
7. Hustawisha mazao mbalimbali, yakiwemo yale yanayohitaji kutuuma kwa maji

